



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA  
WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI



TAARIFA KWA UMMA

MATUMIZI YA MFUMO ULIOBORESHWA WA UTOAJI HUDUMA

Dar es Salaam – 27 Mei, 2026

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), inapenda kuwataarifu wadau wote na umma kwa ujumla kuwa huduma za usajili wa kampuni sasa zinapatikana kupitia mfumo ulioboreshwa wa BRELA Online Service (BOS), unaokusudia kuongeza ufanisi wa utoaji huduma.

Kupitia mfumo wa BOS, mwombaji atajaza taarifa za wakurugenzi, wanahisa na makatibu wa kampuni mara moja tofauti na ilivyokuwa hapo awali. Aidha, mfumo huo umerahisisha utambuzi wa wamiliki wa hisa kwa pamoja (*joint shareholders*), ambapo sasa wana uwezo wa kujaza taarifa zao kwenye mfumo na kutambulika rasmi na Msajili.

Vilevile, wakurugenzi, wanahisa na makatibu wa kampuni sasa wana uwezo wa kuona na kufuatilia shughuli zote zinazoendelea katika kampuni husika. Endapo ombi lolote litaanzishwa na mmoja wao, taarifa kuhusu ombi hilo zitawafikia wote wanaohusika mara tu litakapowasilishwa kwa Msajili.

Kwa upande wa usajili wa mkopo (*charges/debentures*), maombi hayo sasa yatawasilishwa kupitia mfumo wa BOS tofauti na ilivyokuwa hapo awali. Hatua hii itasaidia kurahisisha utoaji wa huduma na kuokoa muda wa wateja katika kuwasilisha na kufuatilia maombi yao.

Aidha, mfumo wa BOS umewezesha wateja kufanya uhakiki wa jina (*name clearance*) kabla ya kuwasilisha maombi ya usajili wa kampuni. Hatua hii itasaidia kupunguza kurejeshwa kwa maombi kutokana na kufanana au kutokubalika kwa majina yaliyopendekezwa kabla ya hatua za usajili kuanza.

Kwa wateja wenye akaunti katika mfumo awali (ORS), wanashauriwa kutumia mojawapo ya njia zifuatazo ili kuingia kwenye mfumo wa BOS:

1. Kutumia anuani ya baruapepe iliyotumika kufungua akaunti katika mfumo wa ORS, kisha kubonyeza kitufe cha "Forget Password", ambapo mtumiaji atapokea baruapepe itakayomwezesha kuingia kwenye mfumo wa BOS; au
2. Kutengeneza akaunti mpya kupitia kitufe cha "Create New Account", ambapo mtumiaji atapokea baruapepe itakayomwezesha kuingia kwenye mfumo wa BOS.

Kwa mteja mwenye maombi yanayoendelea kupitia mfumo wa ORS, ataendelea kukamilisha maombi hayo kupitia mfumo huo mpaka ombi litakapokamilika.

Aidha, maombi yote mapya yanayohusu usajili wa kampuni, mabadiliko ya taarifa za kampuni, uwasilishaji wa taarifa za mwaka (*Annual Returns*), maombi ya kufunga kampuni pamoja na huduma nyingine zinazohusiana, yatawasilishwa kupitia mfumo wa BOS.

Kwa usaidizi wa haraka, tafadhali wasiliana nasi kupitia namba ya simu +255 (0) 22 2212800 au andika kupitia barua pepe [support.bos@brella.go.tz](mailto:support.bos@brella.go.tz)

Imetolewa na;  
**Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma**